

HALMASHAURI YA MJI KIBAHA
Barua zote zipeleklewe kwa mkurugenzi wa mji

S.L.P 30112
SIMU Na: 023 - 2402886
FAX Na: **023 – 240 2007**



OFISI YA MKURUGENZI
MJI WA KIBAHA

TAARIFA KWA UMMA

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Kibaha, Jumatano 03 Februari 2021

Halmashauri ya mji Kibaha katika baraza la bajeti lililoketi leo tarehe 2Februari, 2021 likiongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Mussa Abdallah Ndomba, limepitisha bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kiasi cha shilingi 36,220,091,913.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Akiwasilisha bajeti hiyo kwa umahiri mkubwa, Makamu Mwenyekiti wa halmashauri Mhe. Selina Wilson Msenga amesema katika kiasi hicho mapato ya ndani ya halmashauri ni shilingi 3,937,012,000.00 na ruzuku toka serikali kuu shilingi 31,734,724,263.00 kati ya fedha hizo shilingi 22,237,022,000.00 ni mishahara, shilingi 1,299,312,000.00 ni matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itatumia shilingi 8,198,390,263.00. Aidha, shilingi 548,355,650.00 itatokana na wadau wengine wa maendeleo.

Waheshimiwa madiwani wametoa michango yao ya mawazo na ushauri ushauri ili kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezeka kwa vitendo na kuwaletea wananchi maendeleo. Mhe. Karimu Mtambo, Diwani wa kata ya Picha ya ndege amempongeza Mkurugenzi na wataalam kwa kushirikiana kwenye ukusanyaji wa mapato unapelekea utoaji wa huduma bora kwa wananchi hasa kwenye sekta ya elimu na afya, halmashauri kuendelea kupata hati safi kwa miaka 10 mfululizo huku akishauri kuboreshwa kwa stendi kuu ya mabasi kwa kuweka vivutio vitakavyoichangamsha, kuwaondoa wasioendeleza viwanja eneo la kuzunguka stendi na, kuongeza vyanzo vipya mathalan magulio ya wanyama hai kama mbuzi na kondoo kata ya Pangani vitavyoongoza mapato.

Kwa upande wake, Mhe. Dorice Michael, Diwani viti maalum, amewaomba waheshimiwa madiwani kuwafikia wananchi kutoa elimu ya mikopo inayotolewa na halmashauri (10%) kutokana na mabadiliko ya utaratibu unaoruhusu kutoa vifaa badala ya pesa taslimu kwa baadhi ya miradi inayoombewa fedha kwani wananchi wengi hawana uelewa wa utaratibu huo.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Kibaha mjini Afidu Lwambano akitumia usemi wa watu wa Pwani usemao; *kuvaa dela si kazi, kazi ni kulishikilia* amewapongeza wataalam wa halmashauri kwa kuandaa bajeti nzuri inayoakisi utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 2020-2025 huku akishauri itekelezwa kama ilivyoanisha vipaumbele.

Mkutano huu ulihudhuriwa pia na Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Mhandisi Martine Ntemo na Katibu tawala Sozi Ngate, Wakuu wa Idara na vitengo, wananchi pamoja na waandishi wa habari.

"Kibaha yetu, Maendeleo yetu, Kwa pamoja tunaweza"

Imetolewa na;

Innocent J. Byarugaba
OFISA MAWASILIANO, HABARI NA UHUSIANO